



22140199



SWAHILI A: LITERATURE – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SWAHILI A : LITTÉRATURE – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SWAHILI A: LITERATURA – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Friday 9 May 2014 (morning)

Vendredi 9 mai 2014 (matin)

Viernes 9 de mayo de 2014 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a guided literary analysis on one passage only. In your answer you must address both of the guiding questions provided.
- The maximum mark for this examination paper is *[20 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez une analyse littéraire dirigée d'un seul des passages. Les deux questions d'orientation fournies doivent être traitées dans votre réponse.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[20 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un análisis literario guiado sobre un solo pasaje. Debe abordar las dos preguntas de orientación en su respuesta.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[20 puntos]*.

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi. Ni lazima kuzingatia maswali mawili uliyotolewa kama mwongozo kwenye jibu lako.

1.

Eh! Kiumbe mdogo kama yule! Mbona alikuwa anamshtua wakati alipokuwa na matatizo makubwa ya kufikiria? Isitoshe, Ima aliwachukia panya mno, na kulikuwa na sababu mbili. Kwanza, ni kuwa kila panya alipojitokeza kutoka mafichoni mwake, mamake alimwelekezea yeye lawama kuwa ndiye aliyewavutia viumbe wale kutokana na uchafu aliokuwa nao.

5 Alikuwa ametaka awaangamize kama njia mojawapo ya kuzima ugomvi na mamake. Pili, walikuwa na tabia ya kumshtua wakati alipohitaji utulivu. Ndivyo panya huyu alivyokuwa amefanya wakati huu. Na sasa alikuwa na sababu ya ziada ya kutaka kumwangamiza kwa dhoruba moja, labda ndiyo njia pekee angeondoa hasira kubwa aliyokuwa nayo, hasira iliyoletwa na mawazo mengi kuhusu maisha yake na yale ya mamake. Lakini yule panya aliendelea

10 kusimama pale akiwa anachungulia huku na huku kuona kama kwamba kulikuwa na mtu chumbani. Ima alibaki palepale. Mawazo yakaanza kubadilika. Akamwangalia tena yule panya. “Heri kiumbe kama huyu. Hana fikra zozote. Hasumbuliwi na chochote. Jana na kesho hazimhusu, hazipo katika ulimwengu wake. Tofauti na binadamu ambaye maisha yake daima hunaswa katika mtego wa majuto ya yale aliyoyatenda jana na wasiwasi mkubwa wa yale yatakoyotendeka kesho.

15 Lakini ndiyo maisha ya binadamu, na ndivyo amekuwa tangu jadi. Si mfalme si mtumwa ... sembuse Ima.”

Panya aligeuka polepole na kurudi mafichoni. Japo Ima hakusonga, bila shaka kiumbe huyu mdogo, mwenye ubongo kiasi cha punje ya mahindi aling’amua kuwa kuna mtu kule chumbani na jaribio lolote la kuonyesha umahiri wake katika uwindaji humo chumbani

20 lingekuwa kujitia kitanzi. Si kwamba alifikiria, lakini ndiyo silika waliyoubwa nayo wanyama. Hekima ya kuzaliwa nayo na haihitaji mwalimu wala shule ya kufunzwa. Laiti maisha ya mwanadamu yangukuwa vile.

Lakini kabla ya wazo hili na mseto wa mengine mengi kumkolea akilini Ima alizinduliwa na sauti kubwa mlangoni. Akatanabahi na kusimama ghafla. Bila shaka hakuwa panya.

25 “Yuko wapi huyo hawara? Yu wapi leo nitamla mzima.” Ilikuwa sauti ya mwanamke. “Fungua ama nitaiteketeza nyumba nzima, unasikia Maimuna? Umekula vya bure siku nyingi, leo utalipa.” Aliendelea kupaza sauti huku akiugonga gonga mlango kwa vishindo.

Ima alianza kutetemeka asijue la kufanya. Alikumbuka kuwa mamake daima alimuonya asimfungulie mtu liwe liwalo. Lakini kelele zilizidi. Majirani walianza kufungua milango

30 kutazama kizaazaa kilichokuwa nje. Woga ulianza kumkandamiza Ima. Mara akasikia mlango wa kina Juma umefunguliwa. Bi. Kisauti kama kawaida alikuwa wa kwanza kufoka.

“Taratibu dada kelele za usiku za nini?” Alimwuliza mwanamke aliyekuwa amechemkwa roho si haba. Pumzi zilikuwa zinamwenda mbilimbili huku akila mori nje ya mlango uliofungwa ndi!

35 “Huyu hawara leo atanitambua!” Mama mtu alikuja kwa maneno ya juu kweli. “Eh! Mama mzee badala aolewe yuanyemelea wa wengine. Atakoma. ‘Kisha akarudi kugonga mlango kwa mkono uliokunjwa huku akifoka,’ utakoma wewe kizabizabina, fungua kama wewe ni mwanamke kamili. Mimi nipande wewe uvune siyo?”

40 “Haya basi tumesikia lakini unayemwambia hayuko humu ndani.” Akamjibu Bi. Kisauti. “Jamani utamtoa roho mtoto mdogo aliyepo ndani.”

“Mbona mnanichezea shere lakini, mmeona mie ndiye limbukizeni zaidi asiye na akili hata kidogo? Mimi najua Maimuna amejificha humo ndani na sitaondoka hapa hadi afungue. Hadi afungue.” Alisema huku jasho jembamba likimtoka. “Leo atajua mimi ni sauti binti Daudi.”

45 “Mbona hatuamini jamani? Haya Ima fungua mlango tusije tukaishi hapa nje usiku mzima. Fungua ajionee hakuna mtu atuondokee.” Akashauri mama Juma.

50 Ima alisita kidogo, alikumbuka onyo la mamake. Lakini baada ya mama Juma kumsihi na kumhakikishia kuwa hakutakuwa na tatizo lolote alisalimu amri. Alikuwa karibu kuzirai alipomwona mama aliyejaa ghadhabu na chuki, jadhaba zimempanda kama aliyepagawa. Ilikuwa usiku lakini kwa msaada wa mwangaza mdogo uliokuweco aliona jimama lenye misuli mikubwa na kimo cha kuogofya limesimama kidete huku likihema na kula mori. Macho yalikuwa yamemtoka pima. Hakusubiri kuambiwa karibu. Ghafla bin vuu alikurupuka na kuingia ndani ya nyumba kwa kishindo huku akiangalia na kupekua kila sehemu ya nyumba. Alitupatupa vitu kwa hasira. Si kitanda, si kiti. Hakuna kilichosanzwa.

Joseph Makori, *Ima Fa Ima* (2008)

- (a) Jadili vile lugha inayotumika katika kifungu hiki inavyochangia katika kuendeleza migogoro ya kijamii na kijinsia.
- (b) Jadili maudhui ya kulipiza kisasi katika kifungu hiki na uonyeshe jinsi mwandishi anavyofaulu katika kuyatekeleza akitumia wahusika wake.

2.

Yatima

Ndugu wa kuheshimiwa, bwana usiwe bahati,
Ya maisha maridhawa, japo nafasi ya kati,
Ukawa mwenye ukiwa, wala furaha hupati,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

5 Nakutaka msamaha, usambe ni tashtiti,
Pokea yangu nasaha, shauri nilozatati,
Sikutendei karaha, sikutii kibuhuti,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

10 Kukuomba jambo hili, kwa hii yangu sharuti,
Nakuona yako hali, ulo nao utaiti,
Huna nguvu ilo kweli, za kukabili wakati,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

15 Nikuonavyo yakini, u mgonjwa mahututi,
Mkabla maishani, yakushinda matafiti,
Nakuonea huzuni, na huyu mwana katiti,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

20 Ameachwa ni yatima, mkata si tofauti,
Hana baba hana mama, ila wale afiriti,
Wamfanyia dhuluma, kumpoka pa kuketi,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

Wamemzuia mali, ya babake neemati,
Haki yake ya halali, mashaba ya rutubati,
Amekuwa hana hali, raha pumzi havuti,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

25 Wamemziba pumzi, awe njia ya mauti,
Kuwamithili siwezi, watu hawa laanati,
Katili na tena wezi, waposapo hawajuti,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

30 Kwa hivi langu taraji, lingawa kwako ni uti,
Nataka niwafariji, apendavyo jabaruti,
Huyu mwana mfa-maji, malezi nimdhibiti,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

35 Kwangu usifanye shaka, usiweke kizingiti,
Zaidi ya muafaka, kwako nasema ya dhati,
Kuwa nawe nakutaka, kwenye njema hifadhati,
Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

Ewe mwema mlimwengu, mwenye moyo madhubutu,
Hili ni swali langu, nataka ulipe voti,
Sote tutumai mungu, tumuombe nusurati,
40 Huyu yatima mwanati, nipe nimuonye raha.

Said Karama, *Sanaa Ya Umalenga* (2008)

- (a) Fafanua jinsi mwandishi anavyopitisha ujumbe wake wa ubinafsi na unyanyasaji katika shairi hili.
 - (b) Kwa kuzingatia shairi hili onyesha jinsi mwandishi anavyotumia miundo na mitindo tofauti katika shairi lake na utoe maoni yako kuhusu jinsi anavyofaulu au kutofaulu katika kuyatekeleza haya.
-